



Itakuwaje Kama Una Matatizo au Maswali?

Kama unaona kurudi kwako kazini si kama ulivyopanga, hakikisha mtoa huduma wa afya, mwajiri, na WCB wanafahamu jambo hilo.

Ni kwa namna gani WCB wanashiriki?

- Mwakilishi wako wa WCB atasimamia mpango wa RTW na kukusaidia kama utapoteza mshahara wako.
- Mwakilishi wako wa WCB atakusaidia kama unahitaji msaa katika mpango wako wa RTW - tupo hapa kukusaidia.



Mshirika wa kuaminika, anayehakikisha leo na kujenga kesho iliyo salama.

**Ikiwa utaumia
ukiwa kazini,
tupo hapa
ili kukusaidia.**

Namna ya Kutufikia

Workers Compensation Board of Manitoba
333 Broadway, Winnipeg, MB R3C 4W3

Tutumie barua pepe
wcb@wcb.mb.ca

Kwa taarifa zaidi, tembelea
www.wcb.mb.ca

au tupigie simu
204-954-4321

au simu bila malipo
1-855-954-4321

Ripoti udanganyifu au uzembe

Piga simu 204-888-8081
au piga simu bure 1-844-888-8081
Barua pepe Compliance@wcb.mb.ca

Kazi SALAMA ni jukumu la kila mmoja.
Kuzuia majeraha ni vizuri kwa waajiri na
wafanyakazi. Kwa maelezo zaidi, tembelea kwenye:

safemanitoba.com

au piga simu 204-957-SAFE (7233) ndani ya Winnipeg
au 1-855-957-SAFE (7233) nje ya Winnipeg



**Rudi Kazini
KUPONA
HARAKA**



Ikiwa utaumia
ukiwa kazini,
tupo hapa
ili kukusaidia.

Kurudi Kazini Kunakusaidia Kupona

Kurudi kazini kufuata taratibu za kuumia kazini hatua kwa hatua, kukusaidia baada ya kuumia au kuugua. Cha kwanza kufanya ni kupata huduma za afya zitakazo kusaidia kupona. Kinachofuata ni kupanga lini utarudi kazini kuanza kazi (RTW). Kurudi kazini mapema kimwili na kwa usalama kunaweza kukusaidia kupona.

Mara nyingi, mwajiri wako anapanga hatua za kurudi kwako kazini na mtu anayekupatia kuhuma ya afya. Mwakilishi wako wa umoja/afya na kazi anaweza kujumuishwa, pamoja na mtu wako wa WCB. Mpango utatengenezwa kulingana na mapendekezo ya mtoa huduma na kile unaweza kufanya utakaporudi kazini. Mpango wako wa RTW unaweza kujumuisha mabadiliko ya kazi na kupunguziwa masaa ya kazi.

**Cha kwanza kufanya
ni kupata huduma
za afya zitakazo
kusaidia kupona.**

Faida

Programu ya kurudi kazini inakusaidia:

- kupona haraka na kupona kabisa kutokana na ajali
- kutunza uimara wa kazi yako
- kukusaidia kurudi katika hali ya kawaida na kwa haraka kuliko kawaida kwa baadae.

Ni Namna Gani Unaweza Kushiriki?

- Chukua sehemu ya kazi katika mpango wa RTW wakati wa mjadala wote.
- Hudhuria miadi yako yote ya matibabu na tumia dawa kama ulivyoelekezwa.
- Msaidie mtoa huduma ya afya kutambua kazi unazofanya.
- Kuwa karibu na mtu wako wa WCB na mwajiri wako kujua unavyojisikia, hii inakusaidia kuwa karibu na kazi na kumsaidia mwajiri kukupangia kazi unazoweza kufanya kukusaidia kupona.

Ni kwa Namna Gani Mwajiri Wako Anashiriki?

- Mwajiri wako lazima afanyekazi na wewe na mwajiri wako na mtoa huduma ya afya kutengeneza mazingira ya kurudi kazini kulingana na kile unaweza kufanya.
- Mwajiri wako pia lazima awe karibu na wewe na kukusaidia katika mpango wa kurudi kazini.

Kuajiriwa tena Majukumu?

Sheria inawataka waajiri ambao wana masaa 25 au kuajiriwa au kazi ya muda kuajiriwa upya wafanyakazi majeruhi ambao alikuwa amewaajiri kwa angalau miezi 12 mfululizo kabla ya kujeruhiwa. Kwa taarifa zaidi kuhusu majukumu ya kuajiriwa tena tafadhali angalia kwenye tovuti www.wcb.mb.ca chini ya rasilimali, au piga simu 204-954-4321 au piga simu bure 1-855-954-4321 kupata nakala ya jalida *Majukumu ya Kuajiriwa tena*.

Ni Kwa Namna Gani Mtoa Huduma Wako Anaweza Kushiriki?

- Mtoa huduma wako wa afya anapaswa kupendekeza muda wako wa kurudi kazini na kutoa taarifa za nini unapaswa kufanya.
- Nakala hiyo itaonesha siku unapaswa kurudi kazini kwa usalama na kurekebisha majukumu na masaa unaweza kufanya.
- Mtoa huduma wako wa afya atachangia taarifa za nini hupaswi kufanya kwa mwajiri wako kama utatoa kibali hicho.

